

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**OFISI YA RAISI YA RAISI TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**  
**SHULE YA SEKONDARI LIKAWAGE**

MKUU WA SHULE  
LIKAWAGE SEKONDARI  
S.L.P 195  
KILWA MASOKO  
07/12/2019

KUMB. Na. LIK/SS 2019/12/07  
NDG .....  
SHULE YA MSINGI .....  
S.L.P 04  
KILWA MASOKO

**YAH: MAAGIZO NA MASHARTI KWA MWANAFUNZI ALIECHAGULIWA KUJIUNGA KIDATO  
CHA KWANZA 2020**

Ninayo furaha kukuarifu kuwa umechaguliwa kujiunga na shule ya sekondari Likawage kidato cha kwanza mwaka 2020, shule hii ipo mkoa wa Lindi wilaya ya Kilwa kata ya Likawage kusini magharibi mwa mji wa Kilwa masoko. Shule itafunguliwa tarehe 06/01/2020 saa moja na nusu asubuhi. Sheria namba 25 ya mwaka 1978 itahusika kwa mzazi / mlezi atakaeshindwa kumleta mwanafunzi shuleni kwa sababu yoyote ile.

Mwanafunzi kumbuka kuwa wewe umebahatika kupata nafasi hii nadra uliyopewa na Taifa. Unatakiwa uweke juhudi kubwa katika masomo, kazi, michezo pamoja na mwenendo bora wa tabia kwa manufaa yako na Taifa lako. Unatakiwa kufuata kikamilifu sheria za shule na kanuni zote za shule katika kipindi chote utakapokuwa hapa shuleni.

Masomo unayotakiwa kusoma sekondari ni tisa pamoja na masomo yatakayotolewa na taasisi ya ukuzaji mtaala.

Masomo tisa ya sekondari ni

Civics	Kiswahili	Chemistry
Geography	English	Biology
History	Physics	Basic mathematics

**1.0 MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA ILI MWANAFUNZI APOKELEWE SHULENI**

- A. Nakala ya cheti cha kuzaliwa
- B. Sare ya shule kwa wavulana ni suruali mbili moja ya kaki na nyingine nyeusi, mashati mawili meupe ya mikono mifupi, viatu vya ngozi vya kamba nyueusi jozi mbili pamoja nasoksi nyeupe jozi mbili.
- C. Sare ya shule kwa wasichana ni sketi mbili ya kijani moja na damu yam zee, mashati, soksi ndefu nyeupe jozi mbili

N.B :

- Wanafunzi wa kiislamu wanaruhusiwa kuvaa hijabu nyeupe mahono ya duara usoni isiyo na mapambo au rangi yoyote.
- Viatu na soksi visiwe na rangi, madoa, mistari ya mapambo, pia visiwe na visigino virefu wala mabuti.

- Mwanafunzi haruhusiwi kuvaa kofia, kandambili , pete, herein, n.k. Vile vile haruhusiwi kusuka nywele, kunyoam kipara bila sababu maalumu inayo kubalika na tamaduni za Kitanzania kwa ruhusa maalumu
- D. Shuka mbili za rangi ya blue bahari kwa wavulana na rangi ya pinki kwa wasichana.
  - E. Sweta moja la blue.
  - F. Sare ya michezo kw shule hii fulana nyeupe bukta moja, traksoot ya light blue na viatu vya raba jozi moja.
  - G. Ti –shirt ( fulana) rangi ya zambarau yenye nembo ya shule ambayo ataivaa wakati wa jioni baada ya masomo ya darasani.
  - H. Vifaa vya usafi fagio ya ndani (soft brooms fagio ya nje chelewa), jembe, kwanja, panga ( alete vifaa sio fedha)
  - I. Vifaa vya vya chakula : sahani, kikombe na bakuli, ndoo ndogo mbili
  - J. Viatu vya wazi( ndara) pea moja za kuogea.
  - K. Godoro inch 2½×6
  - L. Picha ndogo nne (passport size) za rangi zenye background blue
  - M. Madaftari makubwa yasiyopungua tisa

## 2.0. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE HII.

Shule inaendeshwa kwa mijibu wa sheria ya elimu Na. 25 ya mwaka 1978. Aidha shule inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara yenye dhamana ya elimu nchini.

Mwanafunzi anatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo :

- a) Heshima kwa viongozi , wazazi, wafanyakazi wote, wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
- b) Mhudhurio katika kila shughuli za ndani na nje ya shule ni muhimu.
- c) Kutimiza kwa makini maandalio ya jioni( preparation)
- d) Kuwahi kaika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
- e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka ya ya shule hivyo wakati wote wa uwanafunzi wako katika shule hii.
- f) Kutunza usafi wa mwili na mazingira ya shule wakati wote.
- g) Kuvaa sare ya shule wakati wote
- h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote.
- i) Mwanafunzi haruhusiwi kutembelea sehemu zifuatazo isipokuwa kwa kibali maalumu
  - i. Chumba cha walimu
  - ii. Ofisi za shule
  - iii. Maabara
  - iv. Jikoni
  - v. Nyumba za walimu na wafanyakazi Wasio walimu
- j) Mwanafunzi haruhusiwi kutembelea sehemu zifuatazo a) vilabu vaya pombe b) majumba ya starehe c) majumba ya kufikia wageni (Guest houses)

### 3.0 MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA SABABISHA UKUFUKUZWA SHULE

- i. Wizi
- ii. Uasherati
- iii. Ubakaji
- iv. Ulevi na matumizi ya madawa ya kurevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, pombe n.k
- v. Kupigana ama kupiga
- vi. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
- vii. Kudharau Bendera ya Taifa
- viii. Kuoia ama kuolewa
- ix. Kupata ma kuharibu mimba ndani na nje ya shule
- x. Kutoa mimba
- xi. Kugoma , kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa shule au watu
- xii. Kukataa adhabu kwa makusudi
- xiii. Mwanafunzi kuwa na simu ya mkononi

### 4.0 GHARAMA ZA HOSTEL (BWENI)

Shule ya sekondari Likawage niya kutwa , shule ina Hostel kwa vijana wa kike na kiume, serikali haitoi chakula kwa ajili ya wanafunzi wanaokaa hostel , gharama za chakula na mpishi kwa wanafunzi wa hostel ni za wazazi.

#### GHARAMA ZA HOSTEL

MUHULA	MICHELE (KG)	UNGA (KG)	MAHARAGE (KG)	SUKARI (KG)	MAFUTA (LITER)	CHUMVI (PAKITI)	MPISHI (TSH)
I	30	30	30	3	3	4	10,000/=
II	30	30	30	3	3	4	10,000/=
JUMLA	60	60	60	6	6	8	20,000/=

### 5.0 FOMU ZINAZOTAKIWA KUJAZWA NA KURUDISHWA SHULENI

- i. Medical examination form ambayo itajazwa na mganga mkuu wa hospitali ya serikali, fomu hii itapelekwa kwa mkuu wa shule iliwa imejazwa.
- ii. Form ya maendelea binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi au mkataba wa kutoshiriki katika mgomo , fujo, ma makosa ya jinai
- iii. Form ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria na kanuni, kumhudumia mwanafunzi kwa mahitaji yote yatakayo hitajika hapa shuleni.

**TAFADHALI SOMA KWA MAKINI MAELEZO, MAAGIZO NA KUYATEKELEZA KIKAMILIFU, NA FOMU ZINZOTAKIWA KUJAZA ZIJAZWE NA ZIRUDISHWE**

KARIBU SANA

.....  
**A.G. MWANDIKE**  
**MKUU WA SHULE**

**OFISI YA RAISI TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**SHULE YA SEKONDARI LIKAWAGE**

**UTHIBITISHO / KIAPO CHA MZAZI / MLEZI**

Mimi ..... Ninakubali mwanafunzi

..... asome katika shule ya sekondari Likawage . Nitahakikisha

kwamba wakati wote mwanafunzi huyu atakapokuwa anasoma hapa shuleni

A} Mwanangu huyu hana ruhusa ya kwenda majumba ya wageni , maeneo ya ulevi, maeneo ya kuangalia sinema na kucheza puul table mtaani. N.K

B} Mimi mzazi /mlezi ninaahidi kumpatia vifaa vyote vinavyohitajika hapo shuleni na ninathibitisha atakuwa na mahali pam kukaa/ kulala muda wote npaka amalize masomo yake

C} Ninaelewa kuwa nafasi hii ya mtoto wangu kuingia katika elimu ya sekondari ni bahati aliyotunikiwa na Taifa kwa jinsi hiyo ninaahidi kuwa nitahakikisha mtoto amafuata sheria na taratibu zote za shule. Pale atakaposhindwa kufuata sheria hatua kali zicchukuliwe dhidim yake

D} Mwanafunzi /mtoto wangu atakapokuwa shuleni alelewe katika dini ya .....

E} ANUANI YANGU .....

F} Saini ya mzazi / mlezi ..... Tarehe .....